JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA

# BARUA YA KICHUNGAJI

## KWA WAUMINI WA MAKANISA YA CCT KUTOKA KWENYE MKUTANO MKUU WA 30 WA JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA WA JULAI 6- 7, 2017

Sisi, Maaskofu na Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania, tuliokutana tarehe 6 hadi 7 Julai 2017, katika Kituo cha Mikutano na Mafunzo cha kumbukumbu ya Askofu Stefano R. Moshi mjini Dodoma, tumepata fursa ya kutafakari majukumu yetu ya Kitume na Kinabii. Kwanza tunawasalimu Wakristo wetu wote kwa jina la Mokozi wetu Yesu Kristo.Mkutano Mkuu unapenda kuleta yafuatayo kama taarifa na kwa ajili ya kuchukuwa hatua zinazostahili.

### 1. UONGOZI MPYA WA CCT

CCT inampongeza na kutoa shukrani za dhati kwa kazi nzuri iliyofanywa na Katibu Mkuu Mchungaji, Dr.Leonard Mtaita aliyetumikia Jumuiya kwa takribani miaka 15 na kwa sasa amestaafu. Pia tunawapongeza Mwenyekiti Askofu Dr. Gehas Alex Malasusa na kamati zote za CCT ambao sasa wamestaafu .Tunampongeza kwa kuteuliwa kwake Mchungaji Kanoni Moses Matonya kuwa Katibu Mkuu wa CCT na kwa Askofu Alinikisa Cheyo kuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania na wajumbe wa kamati mbalimbali. Tunamwomba Mungu awaongoze katika jukumu hili mpya la kuiongoza CCT.

### 2. HALI YA UPATIKANAJI WA CHAKULA NCHINI

Kumekuwa na upungufu wa mvua nchini kutokana na mabadiliko ya tabia nchi. Hali hii imeathiri uzalishaji wa chakula kwenye Mikoa kadhaa na kusababibisha upungufu mkubwa wa chakula kiasi cha kuchochea bei ya vyakula kupanda zaidi ya maradufu. Wananchi katika mikoa mingi wamekabiliwa na upungufu wa chakula na kile kinachopatikana kinauzwa kwa bei ghali. CCT inaiomba Serikali na wadau wengine

wawezeshe usambazaji wa chakula kutoka mikoa yenye ziada kwenda kwenye mikoa yenye uhaba wa chakula ili kuwezesha bei za chakula kushuka kufikia gharama ambayo angalau wananchi wanaweza kupata chakula cha uhakika. CCT inaelekeza makanisa yake kupitia vitengo vya maafa na misaada ya kibinadamu, yaendelee kuwasaidia wananchi kupata chakula kwa bei nafuu kwenye maeneo yao.Pia inawaasa wananchi kutumia chakula kidogo kilichopo kwenye matumizi mazuri na kukihifadhi vizuri. Aidha, makanisa yote yaendelee kumuomba Mungu kwa ajili ya upatikanaji wa mvua ya kutosha na kuhimiza utunzaji wa mazingira, upandaji wa miti kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

## 3. UMOJA WA KITAIFA

Jumuiya inasikitishwa sana na jinsi ambavyo umoja na mshikamano wa kitaifa unavyoendelea kuporomoka. Tunaona migogoro ya ardhi ikiendelea kushamiri, mauaji ya kikatili kwa polisi na raia wilaya ya kibiti,Mkuranga na Rufiji, chuki za kisiasa na uoga wa watu kujieleza ukiendelea kukua miongoni mwa jamii. Hali hii isipotafutiwa ufumbuzi mapema itaendelea kukuza uhasama na kuvuruga umoja wa kitaifa na amani tunayojivunia sasa. Hivyo basi Jumuiya inawataka wakristo wake kuendeleza umoja wa kitaifa na kuendelea kuombea na kuhubiri amani na utengamano wa taifa hili. Pia kuitaka serikali kuchukua hatua za makusudi kutatua migogoro ya ardhi , kutatua migogoro ya kisiasa na kuchukuwa hatua za kudhibiti mauaji,Mkuranga, kibiti na Rufiji. Tunawaomba viongozi wa dini wasimame katika kweli na kuwa nuru ili kuweza kutetea haki na utengamano wa kitaifa.

## 4. MAHUSIANO YA SERIKALI NA HUDUMA ZA JAMII ZINZOTOLEWA NA MAKANISA

Taasisi za kidini zimekuwa na mikataba ya kutoa huduma za afya kwa pamoja na Serikali. Hata hivyo kwa sasa Serikali iko na mipango mikakati mikubwa ya kujenga hospitali zake zenyewe na kuondoa wafanyakazi wa afya wa Serikali walioko katika vituo mbalimbali vya kanisa.Ili huduma hizi ziendelee kutolewa kwa ufanisi Jumuiya inatoa rai ifuatayo;

- Makanisa yaanze kuchukuwa hatua za kujitegemea katika kutoa huduma za afya bila kutegemea Serikali.Kunaweza kuanzishwa kwa Mfuko wa mzunguko wa tiba kwa ajili ya maskini (revolving fund for health for the Poor) kwa ajili ya kutoa huduma za afya kwa watu wasio na kipato.

- Makanisa yachukuwe hatua ya kuwa na ada elekezi katika shule na vyuo vyao zao.Kuhamasisha wakristo kupeleka watoto katika vyuo vya makanisa na kuhakikisha kuwa viwango vya elimu vinavyotolewa katika vyuo hivyo vinakubalika katika soko la ajira.

## 5. ELIMU YA URAIA

Jumuiya inahimiza utoaji wa elimu ya uraia katika makanisa yake yote ili kuwezesha jamii kujua haki zao na pia kuweza kudai haki zao pale zinapokiukwa. Hii ni pamoja na kujua haki zao juu ya kuchagua na kuchaguliwa. Elimu hii iwe endelevu kwa waumini wote wa makanisa wanachama. Hivyo basi, tunahimiza wakristo kuendelea kusoma katiba ya sasa na kujianda kwa mchakato wa katiba mpya pale utakaporudishwa na serekali.

## 6. UVUNAJI WA RASILIMALI ZA NCHI

Kwa zaidi ya muongo mmoja , kumekuwa na malalamiko mengi kuhusu Tanzania kutokunufaika na raslimali za madini yake. Suala hili lilisababisha tafiti mbalimbali kufanywa na watu na taasisi mbalimbali. Ilifanyika mijadala mbalimbali ya ndani na nje ya Bunge, makongamano ya kisomi na mijadala ya taasisi zisizo za kiserikali zikiwepo taasisi za dini kuhusu kutokunufaika na madini yetu. Jumuia ya Kikristo Tanzania (CCT), inapenda kumpongeza Rais kwa kuamua kuchukua hatua kwa ajili ya kurekebisha hali hii.Pia tunalipongeza Bunge kwa kuunda kamati kuchunguza unufaikaji wa rasilimali hizi. . Hata hivyo ili mchakato huu ulioanzishwa na Rais uwe wa manufaa na kudumu zaidi, CCT inamshauri yafuatayo

- Uchunguzi huu usiishie kwenye madini ya dhahabu na gesi tu, uendelee hata kwenye vito vya thamani kama Tanzanite.Tanzania inavito vingi vya thamani ambavyo kama nchi hatujawekeza nguvu kujua ni kwa kiasi gani tunanufaika na vito hivi.Ni vizuri utafiti ukafanywa na hatua za msingi zikachukuliwa.

- Rais akamilishe au aanzishe mchakato wa mabadiliko ya katiba, kama sheria mama ambayo haibadiliki kirahisi. Umiliki na uvunaji wa raslimali za taifa viwe ndani ya katiba kuliko kutegemea utashi wa kiongozi wa nchi. Vipengele vinavyoonyesha umiliki wa rasilimali hizi, ulinzi na matumizi ya rasilimali hizi za umma na vipengele vya uwajibikaji kwa viongozi wote waliopewa dhamana ya usimamizi wa rasilimali hizi viwe ndani ya katiba ili kutowapa viongozi mwanya na uhuru wa kufanya wapendavyo.

## 7. MAOMBI

Maombi ni silaha kubwa ya Wakristo na hii imethibitika wakati kanisa liliposimama kuombea mambo mbalimbali. Tunahimiza Wakristo kuendelea kuombea taifa kuendelea kuwa na amani na utangamano wa kitaifa. Makanisa wanachama wachukue mzigo wa kuombea Taifa angalau mara moja kwa mwezi.

*"Hata hivyo, Bwana anatamani kutupatia neema, anainuka ili kuwaonyesha huruma. Kwa kuwa BWANA ni Mungu wa haki. Wamebarikiwa wote, wanaomgojea yeye"* ( **Isaya 30:18).**

**Imetolewa na**

**MKUTANO MKUU YA JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA**

……………………………………

**Ask. Alinikisa Cheyo Julai 11, 2017**

**Mwenyekiti CCT**